

Kitabu cha Danieli na Ufalme wa Mungu (Kanisa)

DOLA ZA ZAMANI ZA MESOPOTOMIA
NA MEDITERENIA

UNABII WA DANIELI
NA TAFSIRI

DHAHABU

Babeli

(625 K.K. – 539 K.K.)

"Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa cha dhahabu safi ... na Mungu wa mbinguni amekupa ufalme ... Wewe (Nebukadreza wa Babeli) u kichwa kile cha dhahabu."
(Danieli 2:32, 37, 38, pia 1:1)

FEDHA

Umedi–Uajemi

(539 K.K. – 331 K.K.)

"Kifua chake na mikono yake ni ya fedha ... na baada ya zamani zako (Nebukadreza) utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe."
(Danieli 2:32, 39, pia 8:20)

SHABA

Uyunani

(331 K.K. – 63 K.K.)

"tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba ... na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utaitawala dunia yote."
(Danieli 2:32, 39, pia 8:21)

CHUMA NA
UDONGO


Rumi

(146 K.K. – 476 B.K.)

"miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo ... na ufalme wanne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; ...bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu."
(Danieli 2:33, 40, 42, 43)

Ufalme wa Mungu Ulianzishwa (takribani 33 B.K.)

"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele; wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele." (Danieli 2:44).



Agano Jipya linafunua kwamba Yesu na Yohana Mbatizaji walihubiri kuhusu kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu kwa kusema "umekaribia" (Mathayo 3:2; 4:17, 23). Kutokana na kwamba kanisa na ufalme ni kitu kimoja (Mathayo 16:18-19; Marko 9:1; Mdo 1:3; 2:38, 47; 8:12; Wakolosai 1:13), na kanisa lilianzishwa katika karne ya kwanza katika siku za utawala wa dola ya Kirumi, maana yake ni kwamba ufalme wa Mungu ulianzishwa katika karne ya kwanza kutokana na huduma ya duniani ya Yesu. Kanisa/ufalme linaundwa na watu kutoka mataifa yote (Isaya 2:1-2) na hivyo kuziangamiza "falme hizi zote" (Danieli 2:44) na linazungumziwa katika Agano Jipya kwamba lilianzishwa kwenye karne ya kwanza B.K. (Wakolosai 1:13, 2 Wathesalonike 1:5; Ufunuo 1:9). Ufalme huu bado upo leo, na wenye dhambi wote waliotubu wanaweza kuchagua kufanyika sehemu yake kwa kuzamishwa ndani ya Kristo. Yesu, akiwa kichwa cha kanisa lake na Mfalme wa wafalme wote (Wakolosai 1:18; 1 Timotheo 6:15), sasa anatawala katika ufalme wake – watu wake (Mdo. 2:36; Luka 17:21).